(NBAA)

**BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU**

**TANZANIA**

| | | |
|---|---|---|
| SIMU. | (255) (022) 2211890/9 | MHASIBU HOUSE |
| TELEGRAMU: | (255) (022) 2151746 | MTAA WA BIBI TITI MOHAMED |
| BARUA PEPE: | info@nbaa.go.tz | S. L. P 5128 |
| TOVUTI: | www.nbaa.go.tz | DAR ES SALAAM |


NBAA/PR.1/II/61 20th December 2018

# TAARIFA KWA UMMA

## MATOKEO YA MITIHANI YA NBAA ILIYOFANYIKA NOVEMBA 2018

### 1.0 Utangulizi

Katika kikao cha kawaida cha 176 cha Wakurugenzi wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kilichokaa leo Alhamisi tarehe 20 Desemba 2018, chini ya Mwenyekiti wake CPA. Prof.Isaya J. Jairo, kimeidhinisha matokeo kwa watahiniwa waliofanya mitihani ya Bodi iliyofanyika tarehe kuanzia 30 Oktoba hadi 2 Novemba 2018. Mitihani hiyo ilifanyika katika vituo kumi na mbili vya mitihani vilivyopo Tanzania Bara na Visiwani. Mitihani hiyo ilihusisha watahiniwa katika hatua ya Kwanza na ya Pili katika Ngazi ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC I, ATEC II) zenye masomo manne kila moja na Ngazi ya Taaluma; Hatua ya Msingi (Foundation Level) yenye masomo matano, Hatua ya Kati (Intermediate Level) yenye masomo sita na Hatua ya Mwisho (Final Level) yenye masomo manne. Mitihani hii ni ya tisa chini ya mfumo mpya wa elimu na mafunzo unaozingatia weledi.

### 2.0 Matokeo ya mitihani

### 2.1 Matokeo ya Jumla

Watainiwa waliosajiliwa walikuwa **6,802** kati ya hao watahiniwa **619** sawa na asilimia **9.1** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **6,183** sawa na asilimia **90.9**. Kati ya watahiniwa waliofanya mitihani hiyo watahiniwa **217** ambao ni asilimia **3.5** wamefaulu mitihani

katika mkao mmoja, wengine **70** sawa na asilimia **1.1** wamefaulu kwa kufaulu masomo walioyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **928** sawa na asilimia **15.0** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **1,215** sawa na asilimia **17.7** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa wengine **2,228** sawa na asilimia **36.0** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi mbalimbali na watahiniwa **2,740** waliobakia sawa na asilimia **44.3** hawakufaulu mitihani yao.

## 2.2 Watahiniwa waliofaulu kutunukiwa Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC) na Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

### 2.2.1 Cheti cha Utunzaji wa Hesabu (ATEC)

Jumla ya watahiniwa **63** wamefaulu mtihani wa Ngazi ya Cheti (Accounting Technician Level II). Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya Cheti kufikia **3,891** tangu mitihani hii ianze mwaka 1991. Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **21** sawa na asilimia **33.3** na wanaume ni **42** sawa na asilimia **66.7.**

### 2.2.2 Shahada ya Juu ya Uhasibu (CPA)

Jumla ya watahiniwa **371** wamefaulu mtihani wa Shahada ya Juu ya Uhasibu nchini - CPA (T). Kati ya watahiniwa hao wanawake ni **153** sawa na asilimia **41.2** na wanaume ni **218** sawa na asilimia **58.8.** Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani ya CPA kufikia **8,896** tangu mitihani hii ianze mwaka 1975.

### 2.2.3 CPA (T) Mlingano [(CPA(T)] Equivalent

Jumla ya watahiniwa **17** wamefaulu mtihani wa CPA (T) Mlingano [(CPA (T)] Equivalent Qualification Idadi hii inafanya jumla ya watahiniwa waliofaulu mitihani hii kufikia **144** tangu mitihani hii ianze mwaka 2014.

## 2.3 Matokeo katika Ngazi Mbalimbali

### 2.3.1 Ngazi ya Cheti (Accounting Technician)

#### 2.3.1.1 Hatua ya Awali ya Cheti (Accounting Technician Level I)

Katika ngazi ya awali ya mitihani ya Uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC I) watainiwa waliosajiliwa walikuwa **124** kati ya hao watahiniwa **11** sawa na asilimia **8.9** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **113** sawa na asilimia **91.1**. Kati ya watahiniwa **113** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **12** ambao ni asilimia **10.6** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, mwingine **01** sawa na asilimia **0.9** amefaulu kwa kufaulu masomo aliyokuwa ameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **21** sawa na asilimia **18.6** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **34** sawa na asilimia **30.1** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **41** sawa na asilimia **36.3** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **38** waliobakia sawa na asilimia **33.6** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.1.2 Hatua ya Pili ya Cheti (Accounting Technician Level II)

Katika ngazi ya uandishi na Utunzaji wa Hesabu (ATEC II) waliosajiliwa walikuwa **224** kati ya hao watahiniwa **12** sawa na asilimia **5.4** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani katika ngazi hii walikuwa **212** sawa na asilimia **94.6**. Kati ya watahiniwa **212** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **24** ambao ni asilimia **11.3** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **36** sawa na asilimia **17.0** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **60** sawa na asilimia **28.3** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **98** sawa na asilimia **46.2** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **54** waliobakia sawa na asilimia **25.5** hawakufaulu mitihani yao.

### 2.3.2 Ngazi ya Taaluma (Professional Stage)

#### 2.3.2.1 Hatua ya Awali (Foundation Level)

Katika Hatua ya Awali; waliosajiliwa walikuwa **691** kati ya hao watahiniwa **70** sawa na asilimia **10.1** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **621** sawa na asilimia **89.9**. Kati ya watahiniwa **621** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **117** ambao ni asilimia **18.8** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **03** sawa na asilimia **0.5** wamefaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **101** sawa na asilimia **16.3** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **221** sawa na asilimia **35.6** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **236** sawa na asilimia **38.0** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **164** waliobakia sawa na asilimia **26.4** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.2.2 Hatua ya Kati (Intermediate Level)

Katika Hatua ya Kati; waliojisaliwa walikuwa **3,582** kati ya hao watahiniwa **385** sawa na asilimia **10.7** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **3,197** sawa na asilimia **89.3**. Kati ya watahiniwa **3,197** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **33** ambao ni asilimia **1.0** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **56** sawa na asilimia **1.8** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **417** sawa na asilimia **13.0** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **506** sawa na asilimia **15.8** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **1,224** sawa na asilimia **38.3** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **1,467** waliobakia sawa na asilimia **45.9** hawakufaulu mitihani yao.

#### 2.3.2.3 Hatua ya Mwisho (Final Level)

Katika Hatua ya Mwisho; waliosajiliwa walikuwa **2,181** kati ya hao watahiniwa **141** sawa na asilimia **6.5** hawakuweza kufanya mitihani hiyo kwa sababu mbalimbali. Hivyo watahiniwa waliofanya mitihani walikuwa **2,040** sawa na asilimia **93.5**. Kati ya watahiniwa **2,040** waliofanya mitihani katika ngazi hii watahiniwa **31** ambao ni asilimia **1.5** wamefaulu mitihani katika mkao mmoja, wengine **10** sawa na asilimia **0.5** wamefaulu kwa kufaulu masomo waliyokuwa wameshindwa katika mitihani ya nyuma, wengine **353** sawa na asilimia **17.3** wamefaulu mitihani yao kwa kufaulu masomo waliyokuwa wamebakiza. Kwa ujumla watahiniwa **394** sawa na asilimia **19.3** wamefaulu mitihani yao. Watahiniwa **628** sawa na asilimia **30.8** wamefaulu baadhi ya masomo katika ngazi hii. Watahiniwa **1,017** waliobakia sawa na asilimia **49.9** hawakufaulu mitihani yao.

## 4.0 Watahiniwa waliobakiza muhula mmoja kutakiwa kumaliza mitihani yao katika ngazi husika

Wapo watahiniwa 250 ambao walifaulu baadhi ya masomo katika muhula wa Novemba 2016. Watahiniwa hawa wanatakiwa wawe wamefaulu masomo yaliyobakia katika ngazi husika hadi Mei 2019. Hivyo wamebakiza muhula mmoja tu ili kufaulu masomo yaliyobakia la sivyo masomo waliyofaulu huko nyuma yatafutwa na kutakiwa kuanza upya ngazi husika.

## 5.0 Watahiniwa waliofutiwa masomo waliyokuwa wamefaulu

Wapo watahiniwa 393 ambao walifaulu baadhi ya masomo kuanzia muhula wa Mei 2016. Watahiniwa hawa walitakiwa wawe wamefaulu masomo yaliyokuwa yamebakia katika ngazi husika kabla au katika muhula wa mitihani ya Mei 2018. Wanafunzi hawa walishindwa kufanya hivyo na hivyo masomo waliyofaulu yamefutwa na wanatakiwa kujisajili upya kwa ajili ya mitihani hiyo. Hii inajumuisha hata wale ambao hawakufanya mitihani katika muhula huu lakini walikuwa wamefaulu baadhi ya masomo kuanzia Muhula wa Mei 2016 lakini hadi sasa hawajafaulu masomo yaliyobakia.

## 6.0 Pongezi

Bodi inawapongeza wale wote waliofuzu mitihani yao na kuwataka wale ambao hawajafuzu kutokata tamaa bali waongeze bidii zaidi katika masomo yao ili waweze kufanya vizuri katika mitihani ijayo ya Bodi. Bodi inawashauri kutumia vema vitabu vilivyotayarishwa na Bodi katika kijiandaa kwa mitihani yao. Pia wanashauriwa kusoma vitabu vingine vya ziada ili kuongeza ufahamu zaidi katika masomo hayo.

## 7.0 Mitihani inayofuata

- Mitihani ya katikati ya muhula kwa ajili ya somo la Sheria (A5 Business Law), na masomo ya kodi (B4 Public Finance & Taxation I and C4 Public Finance & Taxation II) itafanyika tarehe **Jumanne tarehe 26 na Jumatano tarehe 27 mwezi wa Februari 2019** katika kituo cha Dar Es Salaam tu. Wote wanaopenda kujisajili katika mitihani hii wanakaribishwa.
- Mitihani ya kawaida itafanyika kuanzia jumanne **tarehe 07 mwezi Mei** hadi **tarehe 10 mwezi Mei 2019** katika vituo vitakavyotangazwa.

## 8.0 Uwasilishaji wa picha kwa ajili ya mahafali

Mahafali ya 41 ya NBAA yatafanyika **tarehe 5 mwezi Oktoba 2019**. Tangazo rasmi kuhusu mahafali hayo litawekwa kwenye tovuti ya Bodi. Wale wote waliofaulu mitihani ya ATEC II na CPA (T) pamoja na wale wa CPA (T) Equivalent wanatakiwa kuwasilisha picha zao kwa ajili ya kutengenezewa vyeti kabla ya **tarehe 31 Januari 2019**. Tangazo juu ya namna ya kuwasilisha picha hizo liko kwenye tovuti ya Bodi.

Matokeo haya ya mitihani ya **88** ya Bodi yanapatikana katika tovuti ya NBAA ambayo ni www.nbaa.go.tz

**CPA Pius A. Maneno**
**MKURUGENZI MTENDAJI**